Mungu ndani mwetu



ya Gabriele

Mungu ndani mwetu

Maandishi ya Gabrieli, nabii na mjumbe wa Mungu kwa wakati wetu

First Edition in Swahili: July 2019

1ère édition en Swahili: juillet 2019

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:

Gott in uns (g313sw)

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents

Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés

Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Mungu ndani mwetu

Mada « Mungu ndani mwetu », hususan wakati huu wa sasa, haina maana kwa watu wengi, kwani Tukizingatia matukio inayotangazwa na vyombo vya habari duniani, tutatambua kwamba « Mungu » hapewi umuhimu kama vilevile pia dhamiri ya kuwepo kwake ndani mwetu.

Vyombo vya habari hutangaza kuhusu majanga, mwenendo wa wanadamu, kuhusu mapambano yao wamoja na wengine wakati hawana maoni au dhana moja. Dunia, mazingira yote, wanyama na mimea, vyote huathirika sababu ya utapeli wa « ukristo » usiyo halisi na kwa sababu ya ubinafsi wa wale wanaovitumia. Kila mtu ana hoja zake juu ya uporaji wa dunia, juu ya kuwatesa na kuwaua wanyama na kuharibu mazingira. Hayo yote, bila shaka, hayana uhusiano wowote na Mungu na pia Yesu wa Nazarethi.

Lakini mtu mmoja anajaribu kuthibitisha kwamba: « Mungu yumo ndani mwetu ! »

Inaonekana kwamba wakati huu, watu wengi sana wanajiondoa kwenye makanisa. Mwenendo potovu wa shirika la makasisi unaoripotiwa sana na vyombo vya habari unafumbiwa macho. Unafiki na uongo una-otawala shirika lao vimewekwa bayana, hata pia matendo maovu ya nambari kubwa ya makasisi ambao mwenendo wao wa upotovu unaokithiri, ni machukizo makuu.
Watu hao waliovunjwa moyo hujitenga na kanisa lao, ambamo waliamini watampata Mungu. Wengine husema kwa mashaka:
« Mungu hayupo, kwani Angekuwepo, ni mahali gani alipo sasa ? »
Viongozi vya makanisa hawaaminiwi tena. Wana siasa hurudilia hotuba zao kuhusu « raha kwa watu wote » na « kushughulikia mambo ya jamii », ila tukiangalia kwa undani, tutatambua kwamba yote inalenga manufaa

na raha ya mtu binafsi. Serikali ya Ujerumani inajidai ya kikristo, ila ni muuzaji mkuu wa tatu wa silaha duniani.

Wakati wote ambapo serikali hiyo itaendelea kuwa kibaraka cha tabaka la makasisi na kuigharamia kwa kiwango cha fedha za yuro takriban billioni 14 kila mwaka, hakuna mambo mengi yatakayobadilika kwa sababu, iwe msaidizi anayeshikia kiti mpanda farasi yaani serikali, iwe mpanda farasi mwenyewe, yaani kanisa, hawaoni umuhimu wa kubadili mwenendo wao dhidi ya Mungu na jirani yao. Zaidi ya ruzuku hiyo, ma bilioni ya ziada hutumiwa kama gharama ya ukarabati wa makanisa na makanisa makuu, na fedha hiyo inatoka kwenye mfuko wa serikali yaani kwenye mifuko yetu sisi tunaotoa ushuru.

Ila katika Biblia, ambayo juu yake makasisi wanalia kiapo na ambayo wanaambia waumini wao kwamba ni ukweli kabisa: imeandikwa

kwamba: *« Mungu, aliyeumba dunia na vyote vilivyomo, Yeye, Bwana wa mbigu na dunia haishi katika nyumba iliyojengwa na mikono ya wanadamu. »*
Na sisi, watozwa ushuru, tunapashwa kulipa tena zaidi ushuru. Hivyo basi tutasema tunaacha watunyonyoe manyoa kama kuku, wanatunyonya sana damu, yaani mali, kama wanyama ambao wao wanaishia mateso yao kwenye meza za wakuu wa kanisa.

Hata hivyo, yesu Kristo alisema nini ?
« Wale wote waushikao upanga, wataangamia kwa upanga. »

Vita, mauaji, njaa, mateso, magonjwa, maradhi inayopata watu wengi, ukatili unaotendewa wanyama, vyote hivyo husababishwa kwa sehemu kubwa na binadamu katika ulimwengu tunamoishi.
Ila wanapokabiliana na hali hiyo ya dunia, watu hujiswali: « Mungu yupo wapi ? »

Na wengine husema: « mimi niliamini muda fulani hadithi kuhusu Mungu. Lakini kwa sasa siamini tena. Hakuna Mungu ! »
Je ! Mungu afanye nini na rundo la vifusi ambavyo vimeachwa na ubinafsi wa binadamu ?
Je ! Inambidi abomoe mabaki ya mwisho ? Si lazima afanye hivyo, ni vema mtu ajihusishe mwenyewe na hayo, kwani sisi ndiyo sababu ya hali mbovu hii ya dunia, bali si Mungu !

Marafiki wapendwa, je ! Inawezekana niwaswali swali hili wale walio na uwezo wa kuchambua mambo na wale wasioamini ?
Je ! wewe ni kondoo anayekubali chote wanachomuambia ?
Wewe ni mtu anayeamini yote wanayotaka kumsadikisha, na hata pia kuhusu Mungu, kwa mfano ? Wewe ni kondoo aliye na haja ya makanisa iliyojengwa na mikono ya watu,wewe ni mtu aliye na haja ya desturi, na ya maungamo, na hata pia ya makasisi wanaotegemea kanuni za kanisa na kuzidumisha ?

Ama wewe ni mtu huru, mtu aliyejifunza kufikiri yeye mwenyewe na kutokusadiki yote yanayotumiwa kwa kumdanganya, kwa mfano ahadi kwamba Mungu yupo hapa au kule au pia kwamba machafuko inayotawala dunia hii ni sehemu ya siri za Mungu.

Mimi ni binadamu tu kama binadamu wengine. Mtu anapotoa ahadi ya kitu, angepashwa pia kukihakikisha. Hakuna anayeweza kumhaidi mtu awayeyote kwamba maonyo na mashauri yake ndiyo yatamwezesha kumpata Mungu. Siwezi pia nami kutoa ahadi hiyo. Hatuwezi kupata Mungu hapa au Kule, Mungu ni Uzima ndani mwetu, ndani ya kila mmoja wetu.

Kutokana na asili yetu, sisi ni watu wanaopenda maisha ya kikundi. Hakuna mtu ambaye angepashwa kuwa peke yake kwa maana imeandikwa katika Biblia:
« Si vema mtu awe peke yake ».

Upande mwingine, kutotegemea mtu kunamaanisha kumpata Mungu ndani mwako wewe mwenyewe, kwa sababu kutomtegemea mtu ni msingi wa maisha halisi ya kikundi inayotawaliwa na uaminifu.

Kumpata Mungu kunamaanisha kwanza kujitambua wewe mwenyewe, kufuatana na yale ambayo Yesu Kristo, alifundisha watu, kwa mfano: *« Mimi Kristo ndiye njia, ukweli na uzima. Hakuna ajaye kwa Baba bila kupitia kwangu Mimi ».*

Hayo ni mamoja kwangu pia mimi. Sitegemei mtu yeyote, hata kama ananiahidi mambo mengi na kutaka kunipeleka hapa na pale kwa ajili ya kumpata Mungu.

Hata kama mtu amempata Mungu ndani mwake, hawezi kuyahakikishia wengine. Kuwa na mwenendo mzuri na wa kuigwa ni dalili tu, bali si ushuhuda ulio wazi.

Ndiyo maana kauli yangu haimlazimishi mtu. Maneno yangu yanatokana na mafundisho ya Yesu Kristo, kwa upekee, ahadi aliyotutolea aliposema: « *Mimi ndiye njia, ukweli na uzima* ».

Kile ambacho nilikuwa nategemea na ambacho ninakitegemea tena ni kumpata Mungu. Na nilimpata ndani mwangu mimi mwenyewe kwani sikutegemea mtu. Nilitegemea tu mafundisho ya Yesu Kristo, na ni hayo ndiyo naendelea kufanya.

Katika kitabu kikubwa cha ufunuo wa Kristo « Hili ndilo Neno Langu », tunaweza kusoma ya kwamba, Yesu wa Nazareti alipashwa Naye pia kuwatolea watu wa wakati wake majibu kuhusu Mungu. Imeandikwa hivi katika « Hili ni Neno Langu »:

« Halafu watu wamoja waliojaa mashaka walimjia Yesu wakisema: « ulituambia kwamba eti uzima na maisha yetu hutokana na

Mungu, ila hatujamuona Mungu kamwe na hatufahamu hata Mungu mmoja. Unaweza kutuonesha Mungu; Yule unayemwita Baba na Mungu Mmoja ? Hatujui kwamba kuna Mungu ».

Yesu akawajibu akisema: « Sikilizeni mfano huu juu ya samaki. Samaki wa jito walikuwa wanasimulia kati yao wakisema: Wanatuambia kwamba eti uzima na maisha yetu vinatokana na maji, lakini hatujawahi kuona maji, wala hatujui maji ni nini.

Halafu wengi baadhi yao, wenye akili, kuliko wengine wakasema: Tumesikia kwamba, katika jito mna samaki mwenye hekima na anayejua mambo mengi sana.

Hebu twende tukamwone na tumuombe atuoneshe maji.

Kwa hiyo wamoja wao wakashika njia ya kwenda kumtafuta samaki mkubwa mwenye hekima na wakafika sehemu ya jito ambamo samaki yule alikuwa akiishi na wakamuuliza. Na baada ya kuwasikiliza akawajibu:

« O ! samaki wajinga, wasiofikiri ! Ijapokuwa ninyi ni wenye hekima, wachache wanaotafuta. Mnaishi na kutembea majini ambamo mna uzima wenu. Mulikuja majini na mtarudi majini. Mnaishi ndani ya maji ila hamuyatambui ». Na hivyo ndivyo mnaishi ndani ya Mungu ijapokuwa mnanisihi utuoneshe Mungu. Mungu yumo ndani ya vyote na vyote vimo ndani ya Mungu ».

Kama ilivyo fafanuliwa tayari, mtu hutegemea maisha ya jamii, kutokana na asili yake ya ndani, kwani si vema mtu awe peke yake.
Tukijiunga na Kristo ndani mwetu,Yeye ambaye, katika mafundisho yake alitafuta siku zote na anatafuta tutambue kwamba Yeye ndiye njia, ukweli na uzima, tukiyafuata mafundisho yake hatua kwa hatua, tutaongozwa basi kwenye watu wengine wanaokubali namna yetu ya kuwaza na ya kuishi.

Lakini hatungepashwa kuwategemea.

Tukitoa kauli hiyo inayohakikisha kwamba « Mungu yumo ndani mwetu » inawezekana wamoja wajibu kwamba kufuatana na hali ya jamii yetu leo, kuhakikisha hivyo ni kiburi.

Ila katika Biblia ya makasisi, imeandikwa:
« Lakini Mungu Mkuu sana haishi katika nyumba iliyo jengwa na watu ». Sentensi hiyo husababisha swali hili: ikiwa Mungu haishi katika nyumba iliojengwa na mikono ya watu, je ! Anaishi wapi basi ?

Watu wengi huamini ya kwamba wana nafsi. Tunaweza kuanza kutafakari kama hayo ni kweli au la. Ila Tuanze kutambua kwamba ndani mwetu tuna mwili wa kiroho usio wa dunia hii. Tutambue pia kwamba ndani ya nafsi, mwili wa kiroho, mna Uzima, pumzi ambayo tunasikia katika kupumua kwetu, yaani MUNGU.
Tusidhani kwamba « Uzima » unahusu mwili peke yake, ambao ni ganda la kidunia, yaani

mwanadamu, ambaye siku moja atafariki. Uzima hauna mwisho, ni « Mungu », au « Wa Milele » au tena « Uzima wa milele ».

Tufikirie mazingira: katika majira ya machipuko, nuru huwa kubwa sana na jua huwa kali sana na sehemu ya dunia iliyogeukia upande wa jua huanza kuishi maisha mpya. Mazingira hujivika upya tena rangi yake ya kijani, mimea yote hutoa maua. Ni namna gani kwetu sisi ? Ikiwa tunageukia nuru - Mungu aliye ndani mwetu - nafsi yetu hugeuka yenye nuru; tunaishi kwa dhamiri sana, tunageuka kuwa huru, wenye raha, wakweli, walio wazi, wenye haki kwa jirani yetu, kwa sababu tunajikuta sisi wenyewe ndani ya Mungu, Uzima, na kwamba tuko waaminifu kwetu sisi wenyewe.

Turudilie mada yetu: Mungu ndani mwetu, Mungu ndani mwako, Mungu ndani mwangu. Kila mmjo wetu ni hekalu la Mungu na Mungu anaishi ndani mwetu. Uzima wa mi-

lele ni pumzi ya Mungu iliyo ndani ya nafsi. Uzima unatiririka katika nafsi yetu, unatiririka ndani ya seli za mwili wetu, umo ndani ya kupumua kwetu. Moyo wetu unapiga kwa sababu unapokea Uzima kupitia Uzima ulio pote, Mungu.

Yesu wa Nazareti hakuagiza kamwe kuwepo kwa desturi za makanisa, hakufundisha kwamba tunapashwa kwenda kwenye mahekalu iliyojengwa na mikono ya watu. Yesu alitufundisha na pia aliwaambia makasisi wa wakati wake yafuatayo: « Msiombe watu wawaite Bwana kwani mna Bwana mmoja, yaani Kristo ».

Tunaweza kujiswali bwana yu wapi ? Bwana ni Kristo, ufufuko na Uzima ndani mwetu. Kristo wa Mungu ni Kristo wa Mungu *ndani mwetu*. Yumo ndani mwa Mungu ambaye ni sheria ya upendo na ya uhuru. Ndivyo kila mmoja, hata wewe pia, ni huru kusadiki au kutokusadiki, kujifunga au kujiweka huru.

Sitaki kuwafunga kwa kitu chochote kile au kuwaonesha kitu cha kuwavutia, sitaki pia kulazimisha wengine namna ya kuenenda. Jambo ambalo nigependa tu kuwaambia ni kujaribu nyinyi wenyewe, ikiwa mnataka kufanya yale ambayo mimi na wengine wengi tulijaribu. Kama mimi, walipata Mungu ndani mwao na wamegeuka pia mifano mizuri ya kuigwa.

Imesemeka kwamba Yesu wa Nazareti alifunza watu kuingia katika chumba kidogo mnamo kimya kwa lengo la kumtafuta Mungu katika ukimya. Hakusema kwamba inatubidi kuingia katika makanisa iliyojengwa na mikono ya watu. Je ! Yesu alitaka kusema nini kuhusu chumba kidogo mnamo kimya ?

Kwa mfano nimetengeneza nyumbani mwangu eneo ndogo ya kuombea: nikaweka humo meza ndogo, kiti, na mshumaa. Na jinsi mda ulivyoendelea kupita, kukaa faraghani humo

kukageuka kwangu haja, ninakaa humo kwa ajili ya kuomba ama kusikiliza muziki, kwa ajili pia ya kudumisha kimya ndani mwangu na tena kwa kusali kwa undani na kina.

Hebu, jaribuni nanyi pia, tengenezeni mahali kwenu eneo ndogo pa kuombea. Mfanye kiasi kwamba, kupitia muziki na sala, mahali hiyo iwe na nguvu ya kuwavutia na muwe na dhamiri siku zote kwamba Mungu, Baba yetu wa mbinguni, anawapenda na anatupenda sisi wote. Anahitaji turudi karibu naye, kwani ndani sana ya nafsi yetu, tuko wote wana wa ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu ni nchi yetu ya kweli, isiyobomoka, milele na milele.

Kila mmoja wetu ni huru kuamini au kutoku-amini ya kwamba yeye, kama binadamu msa-firi, ana nafsi ya milele. Nafsi yetu ilijivika kwa muda mwili wa kiutu. Wakati ambapo mwili unakufa, nafsi hufuata njia yake na itaendelea kuifuata hadi muda wa kurudi kwa Muumbaji

wake, Babaye aliye ndani mwake, na kugeuka tena mmoja naye, Kama Yesu alivyosema: *« Baba na Mimi ni mmoja »*.
Umoja huo wa ndani katika Mungu, Baba yetu wa milele, unatuunga sote kama ndugu na dada wa ufalme wa Mungu. Ni nchi ya milele katika Mungu, Baba yetu, inayotuunga.



Tutoe tena maelezo kuhusu chumba chenye ukimya. Mmeelewa hakika kwamba sitaki kuwaelekeza kwenye shirika la nje, kwenye shirika linalotambulika nje. Ninahitaji tu kuhimiza kila mmoja atambue utu wake halisi mwenyewe, kwa kuuliza swali hili: Kwa kweli wewe ni nani au sisi ni nani hakika ?

Ukitaka, tambua wewe ni nani na chambua maana ya maneno haya: Mungu yupo siku zote. Yumo ndani ya mazingira. Yeye ni Uzima, na nuru katika kila mnyama, mmea, kila jiwe, ndani ya kila mti mkubwa.

Mungu yumo ndani ya nafsi yako. Mungu yupo pamoja nawe, karibu nawe, na pamoja na sisi sote.

Wakati unapoingia katika kile chumba kidogo, fanya hayo kwa dhamiri na kitavutia kila mara, hata kama ni nafasi ndogo iliyo kimya. Usiingie na fikra mbaya au ya kiutu ndani ya chumba kidogo hicho ulichokitengeneza kwa ajili ya kuelekeza fikra ndani mwako, na ni muhimu tu kuingia humo wakati unataka kusikiliza muziki au kuomba.

Na wakati unapoomba, elekeza sala zako ndani ya nafsi yako, kwani wewe mwenyewe ni hekalu la Mungu, na Mungu anakaa ndani mwako.



Maelezo hayo hayana lengo la kutangaza mafundisho fulani. Dhamira yangu ni kutetea Mungu, sijitetei mwenyewe wala pia sitetei shirika fulani linalojulikana, ila natetea Mungu peke yake ambaye ningependelea ndugu na dada zangu wajifunze kumjua.

Nimempata Mungu, Uzima, ndani ya nafsi yangu, na ninajua kwamba anatupenda sisi sote. Kama Baba yetu wa milele, alituzingatia na akatuumba moyoni mwake.
Naweza kusema hayo ila siwezi kuyahakikishia mtu. Najua, bila thibitisho ya jambo hilo, kwamba mnaishi milele, kwani Mungu ni Baba yetu. Yeye, Mungu, Baba yetu wa mbinguni alituumba kama viumbe safi vya kiroho.

Siku moja, mwili wetu utakufa, ila wito tunaotolewa na Mungu unabaki na umuhimu wake, wito tunaoutambua pia katika maneno ya Kristo wa Mungu: *« Njoni nyote kwangu, ninyi mliochoka na mlio na mizigo. Nitawatuliza »*.
Tuende wapi kwa kuwa Roho wa Mungu, Kristo wa Mungu, yumo ndani ya nafsi yetu ? Tumuendee Yeye anayeishi ndani mwetu.

Ninazungumza tena kuhusu chumba kidogo mnamo ukimya. Ikiwa unatengeneza mahali kimya pa kuombea na ikiwa unawasha mshumaa na kusikiliza muziki murua kwa ajili ya kutambua utu wako, utahisi kwamba hauko peke yako. Kuna kitu ndani mwako kinachozungumza nawe, kinachokuhimiza, kinachotaka kukuelekeza na kukuongoza.

Kuna swali ambalo kila mtu analojiswali siku zote: namna gani kumkaribia Mungu kusudi ya kurekebisha vema utu wetu, hata namna yetu yote ya kuishi. Tukiwa na haja hiyo ndani ya moyo wetu, tutakumbuka kwamba Mungu alitutolea misaada na mashauri kwa kufikia kurekebisha vema utu wetu. Mungu, Baba yetu wa milele, alitutolea kupitia Musa, Amri kumi, na kupitia Yesu, Mafundisho ya Mlimani.



Mchambuzi mzuri anaelewa maana ya amri kumi za Mungu na Mafundisho ya Yesu Mlimani, na anatambua ya kwamba wakati mpya unakuja hima. Unakuja. Wamoja wanataka kugeuka watu wapya, watu huru, wanaoishi ndani ya Roho wa Mungu, wanaoheshimu na kupenda mazingira, wanaoishi na majirani wao kwa amani, kwa nguvu ya Mungu. Hivi ndivyo watu wa wakati mpya, vizazi vya siku zijazo watakavyoishi.

Je ! Unakubali kufuata njia hiyo ? Kwa hiyo hauhitaji kiongozi cha nje, kwani Kiongozi cha ndani, Kristo wa Mungu yumo ndani mwako. Yuko ndani ya kila mmoja wetu.

Jaribu kujitambua mwenyewe ili ukaribie Uzima wa halisi. Hakuna aliye na ruhusa ya kukulazimisha utekeleze yale ambayo Roho anaagiza. Katika Roho wa ukweli, katika Mungu, sisi sote tu watu huru.

Lakini inaruhusiwa kutoa ushuhuda, sasa napenda kushuhudia:

Ninampenda Mungu, Baba yetu wa mbinguni, kwa sababu nilitambua kwamba anawapenda, anatupenda sote.

Hatuna haja ya makanisa, hatuhitaji desturi za makanisa, makasisi, mpatanishi kati yetu na Mungu. Kwani tuna kitu cha thamani ndani mwetu, kitu cha thamani mno. Yesu, Kristo, anatuomba tuchimbue hazina hiyo iliyo ndani mwetu, kwa sababu anatufundisha: *« Mimi ni njia, ukweli na uzima »*. Anatuhimiza akisema: *« Mnifuate »*.

Nilisafiri kwa ajili ya kukaribia hazina hiyo ya kiroho, na siongei kuhusu kitu ambacho sikujaribu. Ninaongea kutokana na uzoefu nilio nao, na ninajua kwamba mnaweza kuchimbua hazina hiyo, na sote tunaweza kufanya hivyo.

Nitakuwa na raha ikiwa mnaanza safari ya kwenda kutafuta hazina hiyo ipitayo vyote.

Nitakuwa mwenye furaha mkipata amani ya ndani, kwa sababu mna dhamiri kwamba Mungu yupo.

Nitafurahi mkihisi kwamba ninyi si peke yenu na kwamba ndani mwenu mna kitu kinachojionyesha, kinachopumua, mna wimbi linalotiririka. Ni Roho, ni Ukweli, Uzima ulio ndani mwenu na ndani ya kila mmoja wetu.



Ninawatakia mpate chumba hicho kidogo mnamo kimya.

Ninawatakia muombe kwa undani na bidii.

Ninawatakia kukua katika uhuru.

Ninawatakia muishi ndani na pamoja na mazingira.

Ninawatakia muwasiliane na Roho wa Mungu aliye ndani mwenu na ndani ya jirani wenu.

Katika dhamiri hiyo, nawatolea salamu ya furaha katika Mungu, nikiwaambia: Mungu yu pamoja nasi !

Gabriele

Spiritual Books To Learn From,
and Attain Ethical Moral Values

Des livres spirituels pour apprendre !
Développer des valeurs éthiques



Learn to Pray


In True Prayer You Experience God,
True Prayer Makes You Happy

60 pages

Apprends à prier

Dans la prière véritable tu fais l'expérience de Dieu. La prière véritable te rend heureux

54 pages



The Ten Commandments of God through Moses

Interpreted with present-day words

44 pages

Les Dix Commandements de Dieu donnés à travers Moïse

Expliqués dans le langage d'aujourd'hui

44 pages

www.gabriele-publishing.com

Free Brochures / Brochures gratuites



Message of Truth

- Find God. Where? How?
- Reincarnation – Life's Gift of Grace
- Don't Let Go!
- Comfort in Need and Suffering
- A fulfilled Life Into Old Age

Le message de la vérité

- Dieu en nous
- Des perles de vie
- Vous n'êtes pas seul
- Vous vivez éternellement, la mort n'existe pas
- Le Sermon sur la Montagne, la clé d'une vie intérieure riche

Kitabu katika lugha ya Kiswahili kinachotelewa bila malipo:

- Usikate tamaa! Stahimili!



Info at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05

Mungu ndani mwetu

ya Gabriele

Dhamira yangu ni kutetea Mungu, sijitetei mwenyewe wala pia sitetei shirika fulani linalojulikana, ila natetea Mungu peke yake ambaye ningependelea ndugu na dada zangu wajifunze kumjua.
Nimempata Mungu, Uzima, ndani ya nafsi yangu, na ninajua kwamba anatupenda sote, kama Baba yetu wa milele, alituzingatia na akatuumba moyoni mwake.
Mungu yupo daima. Yupo katika mazingira. Mungu ni Uzima, ni nuru, iliyo ndani ya kila mnyama, kila mmea au kila jiwe, ndani ya kila mti. Mungu Yumo ndani ya nafsi yako. Yupo pamoja nawe na Yupo kando yako.

Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany

www.gabriele-publishing.com